East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 4, Issue 1, 2019
ISSN: 1476-4687

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

Original Article

# MATUMIZI YA RIWAYA KATIKA KUTOA MUKTADHA WA UFAFANUZI WA MUUNDO WA SENTENSI KATIKA SHULE ZA UPILI, KAUNTI NDOGO YA WEBUYE MAGHARIBI

*Elizabeth Nakhumicha Soita*, Dkt. Edwin Masinde, Dkt. Ben Nyongesa*

*Chuo Kikuu cha Kibabii, S.L.P 1699 – 50200, Bungoma, Kenya, elizabethsoita2014@gmail.com

**Article history:**

*Received: 07 Jul 2019*
*Accepted: 18 Jul 2019*
*Published: 26 Jul 2019*

**Keywords**:

*Mwelekeo Mseto,*
*Usetaji,*
*Fasihi,*
*Lugha,*
*Riwaya,*
*Muundo wa Sentensi*
*Utekelezaji.*

## IKISIRI

Kwa muda mrefu mafunzo ya lugha na fasihi yamekuwa yakitengwa ingawa silabasi ya K.I.E. (2002) ilipendekeza mwalimu anapofundisha atumie mwelekeo mseto kwa sababu silabasi hii iliorodheresha tu mada za fasihi na lugha bila kutoa mwelekeo wa utekelezaji. Hali hii ilimpa mtafiti msukumo wa kufanya utafiti kuhusu matumizi ya riwaya katika kutoa muktadha wa ufafanuzi wa muundo wa sentensi katika shule za upili, kaunti ndogo ya Webuye Magharibi. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuonyesha matumizi ya riwaya katika kutoa muktadha wa ufafanuzi wa muundo wa sentensi na utekelezaji wake shuleni. Nadharia jumuishi ya ufundishaji wa lugha iliyoasisiwa na Hammerly (1985) ilitumika katika utafiti. Muundo wa usoroveya-elezi ulitumika katika utafiti huu. Shule 17 zilifanyiwa utafiti. Idadi ya walimu 35 na wanafunzi 43 walitafitiwa. Deta ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya hojaji, mahojiano na utathmini wa maazimio ya kazi, mipangilio ya masomo na mitihani. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa riwaya inaweza kutoa muktadha wa ufafanuzi wa muundo wa sentensi ingawa changamoto ni kuwa asilimia 68.57 ya walimu hawakutambua pendekezo la silabasi ya K.I.E (2002) la ufundishaji wa mwelekeo mseto. Walimu 11 (31.43%) walikuwa na ufahamu wa kuseta. Walimu 7 kwa 11(63.63%) walipata ugumu wa kutekeleza ufundishaji mseto. Walimu 4 kwa 11 (11.43%) walifundisha riwaya pamoja na muundo wa sentensi wala si kufundisha muundo wa sentensi kwa kutumia riwaya. Walimu 31 kwa 35 ambao hawakuzingatia mwelekeo mseto katika ufundishaji wa muundo wa sentensi kwa kutumia riwaya walionyesha uwezekano wa riwaya kuweza kutumika kufundisha muundo wa sentensi. Mtafiti alipendekeza walimu wahamasishwe kuhusu utekelezaji wa mwelekeo mseto wa fasihi na lugha darasani ili kuboresha lugha kwa ujumla. Kwa mujibu wa utafiti huu, vitabu vya riwaya vinapaswa kuteuliwa kwa uangalifu ili viwe na manufaa kwa ufundishaji wa muundo wa sentensi.

## UTANGULIZI

Ufundishaji mseto ulitokana na mtazamo wa wanamaendeleo wa elimu kama vile John Dewey, Maria Montessori (1948), Jean Piaget (1952) na wengineo. Dewey (1938) alisema kuwa masomo yote yanatokana na dunia moja na uhusiano katika maisha na hivyokunapaswa kuwe na umoja wa kiasili katika masomo. Kulingana na falsafa ya Dewey (k.h.j), anapendekeza usetaji katika ufundishaji kwa manufaa ya wanafunzi. Dewey (k.h.j) akinukuliwa na Schiro (2013) kwamba walimu wanapojiandaa kufundisha, ilhamu ya wanafunzi inapaswa kuzingatiwa na masomo ya mtaala yaweze kusetwa huku wakizingatia ujifunzaji mradi. Elimu ya jadi ilichukuliwa kuwa ya kutovutia na ya kuchosha kwa vile mazingira hayakuchochea ujifunzaji (Brendto, 1999). Aidha, elimu ya jadi ilizuia mchangona ubunifu wa wanafunzi. Isitoshe, ili wanafunzi kutia bidii, walimu walitegemea thawabu au adhabu kulazimisha wanafunzi kumakinika na kujifunza. Montessori (2013) aliamini kuwa mbinu ambayo ingelenga ilhamu ya wanafunzi ingefanikisha ujifunzaji.

Graham (2007) akiunga mkono mtazamo wa Dewey (k.h.j) anasema elimu inastahili kwa kawaida isetwe na mbinu za ufundishaji ziwe halisi na isiwe ya darasani tu bali iruke mipaka na kuhusisha mambo mbalimbali ya maisha. Anasema lengo mojawapo ya ya elimu ni kujenga uhusiano miongoni mwa wanafunzi na wanafunzi na jamii. Anaongezea kuwa elimu inapohusishwa na tajriba ya ulimwengu halisi, wanafunzi wanaweza kulinganisha maswala ya kitamaduni, ya kisiasa na ya kijamii. Kwa jumla, hawa wanamaendeleo wa elimu wanasisitiza usetaji wa masomo huku ilhamu na mbinu mwafaka zikitumiwa na masomo hayo yaguzie mambo yaliyomo katika ulimwengu halisi ili elimu isifae tu wanafunzi darasani bali wawe wazalendo.

Kutokana na mawazo haya ya wanamaendeleo wa jadi na tafiti ambazo zimefanywa kwa muda mrefu katika nchi mbalimbali kuhusu usetaji wa masomo na kuonyesha ufanisi. Ripoti ya Koech (1999) ilipendekeza usetaji wa kikamilifu ilikupata elimu na maandalizi bora (TIQET). TIQET ilishikilia ufunzaji wa kijumla wa masomo wala si kugawanywa katika sehemu teule ya kitaaluma. Hali hii ililenga mwelekeo mseto waufundishaji katika somo la Kiswahili katika shule za upili hasa lugha na fasihi. Mapendekezo haya yaliipa Taasisi ya Elimu msukumo wa kuandaa silabasi ya K.I.E (2002) iliyopendekeza ufundishaji mseto wa fasihi na lugha katika ufundishaji kutokana na manufaa yake makubwa.

Kutokana na msisitizo huu kuhusu ufundishaji mseto wa fasihi na lugha na Taasisi ya Elimu kutotoa mwelekeo kuhusu utekelezaji wa ufundishaji mseto, mtafiti alipata ilhamu ya kufanya utafiti kuhusu matumizi ya riwaya katika kutoa muktadha wa ufafanuzi wa muundo wa sentensi. Mtafiti alitumia riwaya ya *Kidagaa Kimemozea* na *Chozi la Heri* kama vielelezo vya riwaya.

Malengo ya utafiti huu ni kuonyesha matumizi ya riwaya katika kutoa muktadha wa ufafanuzi wa muundo wa sentensi na kubaini utekelezaji wa mwelekeo mseto katika ufundishaji wa muundo wa sentensi kwa kutumia riwaya.

## NADHARIA YA UTAFITI

Utafiti huu uliongozwa na nadharia jumuishi ya ufundishaji wa lugha iliyoasisiwa na Hammerly (1985). Nadharia hii inashadidida kuwa umilisi wa stadi tofauti za lugha ni muhimu kwa uimarishaji wa lugha kwa jumla. Stadi hizi ni kama vile stadi za kiisimu ambazo ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika; stadi za utambuzi wa maarifa; stadi za kutambua hisia na mielekeo ya binadamu na mwisho kuna stadi za njia, mbinu na mikakati ya ufundishaji. Aidha, nadharia hii huhitaji mwalimu na mwanafunzi wawe na maarifa kutoka nyanja tofauti kama vile saikolojia, filosofia na anthropolojia. Nadharia hii inashikilia kuwa ufahamu wa saikolojia ni muhimu katika kubainisha tabia zinazohusiana na ufundishaji lugha. Anthropolojia inahusiana na kubainisha asili ya lugha na mabadiliko yake. Filosofia nayo huchunguza sababu za kuibuka kwa lugha katika jamii. Isitoshe, nadharia hii huchukulia kuwa ni muhimu mwalimu anapofundisha azingatie maarifa awali walionayo wanafunzi ya umilisi wa utamaduni, umilisi wa mawasiliano na umilisi wa kiisimu. Umilisi wa utamaduni huhusu uhamasisho wa mielekeo, maarifa na stadi katika utamaduni wa lugha. Opunde (2012) akimnukua Hymes (1972)

anasisistiza kwamba umilisi wa mawasiliano utasaidia wanafunzi kuweza kutagusana darasani. Umilisi wa kiisimu huhusu utambuzi wa utamkaji wa sauti katika lugha, ufahamu wa maumbo ya maneno, miundo ya sentensi, maana inayojitokeza katika maneno ya sentensi na matumizi katika miktadha mbalimbali.

Nadharia hii inafaa utafiti huu unaohusu matumizi ya riwaya katika kutoa muktadha wa ufafanuzi wa muundo wa sentensi. Umilisi wa kiisimu utasaidia mwalimu kuwa maarifa ya miundo mbalimbali ya sentensi. Maarifa ya utamaduni yatasaidia mwalimu kufahamu maarifa awali ya wanafunzi na kuweza kuwasaidia kumudu kanuni za lugha ya Kiswahili. Umilisi wa mawasiliano utasaidia wanafunzi waweze kutagusana darasani nayo maarifa ya kisaikolojia yatasaidia mwalimu kutambua hisia na mielekeo ya wanafunzina kutambua mbinu mwafaka ya ufundishaji ili wanafunzi waweze kuwa na hisia na mielekeo chanya katika somo.

## UHAKIKI WA MAANDISHI

### Dhana ya Fasihi

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), fasihi ni sanaa inayotumia lugha ambayo hujishughulisha na binadamu pamoja na maisha yake na huathiri, hugusa au huacha athari fulani na hupatikana katika umbo ambalo linatambuliwa na jamii fulani. Kwa hivyo, fasihi ni sanaa inayotumia lugha kuwasilisha ujumbe unaomhusu binadamu na maisha yake.

### Dhana ya Riwaya

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), riwaya ni hadithi ndefu ambayo in visa na vitushi, migogoro na inayosimulia mambo yanahusiana na jamii. Kwa mtazamo wa mtafiti, riwaya ni hadithi ndefu za kubuni zinazotumia lugha ya nadhari kusimulia maisha ya binadamu; shughuli na migogoro yao.

### Dhana ya Lugha

Lugha ni chombo cha kuwasiliana kwa binadamu wa utamaduni wa aina moja au tamaduni mbalimbali, ikiwa watajifunza. Mawasiliano kati ya watu hawa yanazingatia mambo ya msingi; yakiwemo matumizi ya alama fulani ambazo huandamana na sauti ananena Mbunda (1992) akinukuliwa na Matinde (2012). Mtafiti naye anasema kuwa lugha ni mfumo wa sauti nasibu zenye maana zinazotumiwa na binadamu wa tamaduni fulani katika mawasiliano.

### Dhana ya Mwelekeo Mseto Katika Ufundishaji

Mwelekeo mseto niufundishaji ambao umepangwa kwa mtindo ambao masomo tofauti yaliyo na uwiano fulani hujumuishwa na kuchangiana na kufanya ufundishaji kuwa bora licha ya upana wake (Shoemaker, 1989). Pia, usetajini kuleta pamoja masomo tofauti yenye uhusiano fulani ili kusuluhisha matatizo ya maisha au masomo mapana ambayo mada mbalimbali hujumuishwa iliufundishaji uwe bora (Good, 1973). K.I.E (2006) nayo inaeleza kuwa mwelekeo mseto katika muktadha wa ufundishaji wa lugha na fasihi una maana ya kuwa matini ya fasihi zinatumiwa kama dafina na chemichemi ya kufunzia lugha hasa sarufi. Maelezo haya yanafaa utafiti huu.

*Ngazi za za Mwelekeo Mseto (Usetaji)*

Usetaji unaweza kutumika katika uwanja mmoja au zaidi. Huu ni mtazamo ambao umekubaliwa na wasomi mbalimbali kwa msingi kuwa tajriba ya maisha hutoa maoni kuwa suluhu ya matatizo ya maisha haipatikani katika usomaji wa kutenga masomo (Aina, 1979). Lewey (1991) akinukuliwa na Mamai (k.h.j) anasema usetaji katika mtaala kwa desturi hufuata mojawapo ya mitindo mine. Kwanza, uwiano wa nyanja mbili au zaidi za mafunzo ya taaluma moja; pili, usetaji katika uwanja mmoja mpana wa mafunzo; tatu, usetaji unaohusu maeneo ya taaluma tofauti zenye kuingiana; na nne, usetaji wa uwanja mpana wa mtaala. Silabasi ya K.I.E (2002) inapendekeza usetaji wa uwanja mpana wa mafunzo na usetaji wa nyanja mbili au zaidi za mafunzo katika taaluma moja.

*Usetaji Katika Uwanja Mmoja Mpana wa Mafunzo*

Usetaji katika uwanja mmoja mpana, maswala mawili au zaidi hufungamanishwa katika uwanja wa mafunzo, anena Broudy (1964) akinukuliwa na Mamai (k.h.j). Kuhusu hii ngazi, K.I.E (2002) inasema kuwa mwalimu anapofundisha somo kama vile sarufi, ajaribu kujumuisha stadi zingine za lugha katika kipindi hichohicho.

*Uwiano kati ya Nyanja Mbili au Zaidi za Taaluma Moja*

Uwiano katika nyanja mbili au zaidi unamaanisha nyanja mbili za mafunzo kufundishwa pamoja ili mafunzo hayo yachangiane na kujenga ufunzaji katika uwanja mwingine. Katika hii ngazi, silabasi ya K.I.E (2002) inasema kuwa masomo ya lugha na fasihi yachangiane. Yaani mwanafunzi anapozingatia fasihi atumie matini ya fasihi kama muktadha wa kufafanua vipengele vya sarufi, msamiati, istilahi na vipengele vinginevyo. Utafiti huu umezingatia hii ngazi ambapo riwaya inachangia ufundishaji wa muundo wa sentensi.

**Uhusiano Kati ya Fasihi na Lugha**

Fasihi na lugha hutegemeana. Shang (2006) anasema kuwa lugha na fasihi haviwezi kutenganishwa kwa sababu yote hukuza ujifunzaji ukawa bora. K.I.E (2006) inaeleza kuwa lugha ndicho chombo muhimu cha kuwasilishia na kufunza au kujifunza fasihi. Bila lugha, haiwezekani kutenda, kufafanua, kuhakiki au kuelewa kazi za fasihi.Yaani, bila lugha hakuna fasihi. Kwa upande mwingine, bila fasihi, lugha itakuwa chapwa, kavu na na iliyokosa ladha, mvuto na mnato unaopendeza na kuchangamsha mwanadamu.

**Umuhimu wa Usetaji wa Fasihi na Lugha**

Silabasi ya K.I.E (2002) inatilia mkazo matumizi ya mwelekeo mseto wa kujumuisha lugha na fasihi ili masomo haya mawili yachangiane. Vipindi vya lugha huwasinya wanafunzi kwani huwa vikavu na wanafunzi huelekea kuvichukia kwa upande mwingine, wanafunzi huvipenda na kuvichangamkia vipindi vya fasihi. Kwa hivyo, ufundishajiwa sarufi na matumizi ya lugha unaweza kupata uhai na mvuto ukiegemezwa kwenye fasihi. Fasihi itaweza kutumika kama msingi wa kusaidia wanafunzi kuvimudu vipengele vya sarufi, kuendeleza na kuimarisha ujuzi wa lugha na kupanua msamiati wao. Vile vile, wataweza kutambua uhusiano ulipo katiya lugha na fasihi. Isitoshe, jambo hili litaweza kuwapa nafasi ya kuona namna lugha inavyotumika katika utendaji. Mathalani kusimulia tukio, kuelezea mhusika, kutumia tamathali za semi, kufupisha na kadhalika (K.I.E, 2006). Madai haya yameungwa mkono na Mckay (1982) na Brumfit (1985).

Aidha usetaji wa fasihi na lugha kando na kusaidia wanafunzi kukuza msamiati na sarufi, husaidia katika kutambua muundo wa aya na kupata ujuzi wa kuwasiliana na kupata maarifa ya aina na mitindo ya kuandika. Licha ya hayo, fasihi husaidia mwanafunzi kutumia maarifa yake awali katika ujifunzaji wa maarifa mapya (Brinton na wengine, 1989) akinukuliwa na Shang (2006). Erkaya akinukuliwa na Shang (k.h.j) anasema kuwa usetaji wa fasihi na lugha husaidia katika kukuza stadi zote nne za lugha; kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Kwa njia bora zaidi kutokana na uhalisia, tafakari ya hali ya juu na wanafunzi kuvutiwa na somo. Shang (k.h.j) alimnukuu Abulhaija (1987) akiunga mkono kuwa lugha na fasihi haziwezi kufundishwa kwa kuzitenga kwa sababu huchangiana ili mwanafunzi aweze kufahamu somo vizuri (taf).

Mafunzo ya sarufi huwajuza wanafunzi kanuni za lugha ambazo huwawezesha kuchunguza matumizi ya lugha katika kazi ya fasihi (Odeo, 2006) akinukuliwa na Opunde (k.h.j). Juu ya hayo, usetaji wa lugha na fasihi huwapa wanafunzi fursa ya kutumia uwezo wao badala ya kutegemea utahini wa kuandika na wa midomo (Pidgon na Woolley, 1992). Wanafunzi hupewa fursa ya kutagusana na kuwasiliana na wenzao hivyo kuweza kutambua maarifa kivyao huku wakielekezwa na mwalimu.

Matini ya fasihi yana miktadha mingi muhimu ambayo mambo mbalimbali kuhusu lugha kama vile vipashio vya lugha na muundo wake hutumika kwa njia ya kawaida (Brumfit na Cartel, 1986). Fasihi huchukuliwa kama nyenzo ya kufanya wanafunzi wakuze utambuzi wa mifumo ainati za lugha. Licha ya hayo fasihi huweza kuboresha ufasiri wa wanafunzi na kuinua kiwango chao cha lugha na ujuzi wa mawasiliano. Fasihi ni halisi na ina uwezo wa kuchangia ufundishaji wa lugha (Ghoshen, 2002; Shrestha, 2008 wakinukuliwa na Khatib, Rezaei na Derakhshan, 2011)

Kwa jumla usetaji wa fasihi husaidia mwanafunzi kuchangamkia lugha, kukuza sarufi na msamiati na vile vile stadi za lugha. Hivyo basi, utafiti huu wa kutumia riwaya katika kutoa muktadha wa ufafanuzi wa muundo wa sentensi utakuwa wenye

manufaa makubwa katika ufundishaji na hata ujifunzaji.

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti ulifanywa katika kaunti ndogo ya Webuye Magharibi katika kaunti kuu ya Bungoma. Sababu ni kuwa eneo hili lilikuwa na takribani shule za kategoria zote. Aidha, mtaala wa shule zote za upili ni sawa nchini kote na eneo hili lilitumiwa kama eneo akilishi. Isitoshe, shule za eneo hili zimekuwa zikishuhudia matokeo mabaya hasa kwa mtihani wa Kiswahili wa kitaifa. Kwa mfano mwaka wa 2016-2017 matokeo ya Kiswahili yalikuwa 3.273(D), 3.462 (D) na 3.778 (D+) mtawalia (ripoti ya K.N.E.C, 2018). Mtafiti alitumia muundo wa usoroveya elezi kwa vile unafaa watu ambao wana uzoefu wa tatizo linalochunguzwa na wanaweza kuchangia mambo muhimu (Kothari, 2003). Eneo hili lilikuwa na jumla ya shule 36. Shule 17 zilihusishwa katika utafiti. Usampulishaji wa shule ya kitaifa za kiwango cha juu za kaunti na za kibinafsi ulikuwa wa kimakusudi kwa vile zilipatikana kwa uchache na uteuzi wa shule za kiwango cha chini za kaunti (30%) kulingana na Kothari na Garg (2014) ziliteuliwa kinasibu kwa vile zilipatikana kwa wingi. Mtafiti alinuiia kuteua walimu wote wanaofundisha kidato cha tatu kimakusudi ili kuafitki malengo yake. Uteuzi wa wanafunzi ulikuwa wa kinasibu. Mwanafunzi mmoja mmoja kwa kila mkondo aliteuliwa kwa vile mafunzo ni sawa. Mtafiti alikusanya deta kupitia maswali ya mahojiano, hojaji, maazimio ya kazi, mipangilio ya masomo na tathmini ya mitihani. Deta iliwasiliswa kwa kutumia maelezo, asilimia na jedwali.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Riwaya kama Muktadha wa Ufafanuzi wa Muundo wa Sentensi

Madhumuni ya kwanza yalikuwa kuonyesha matumizi ya riwaya kama muktadha wa ufafanuzi wa muundo wa sentensi katika shule za upili. Ili kuonyesha riwaya kama muktadha wa ufafanuzi wa muundo wa sentensi, mtafiti alionyesha virai, vishazi na aina za sentensi katika riwaya. ya *Kidagaa Kimemwozea* na *Chozi la Heri*. Mtafiti alitumia hizi riwaya kwa vile zina miundo anuai za sentensi. Aidha riwaya hizi ziko katika kiwango cha wanafunzi.Isitoshe, matumizi ya riwaya mbili ni ishara kuwa riwaya zozote zile tuele zaweza kutumiwa kufundisha lugha.Ifuatayo ni mifano ya miundo ya virai, vishazi na aina za sentensi kutoka kwa riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na *Chozi la Heri*.

*Virai*

Kirai ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina muundo wa kiima na kiarifa (Wamitila, 2005). Aidha kirai ni sehemu ya sentensi inayojengwa kwa neno moja au zaidi yasiyojumuisha kiima na kiarifa. Kuna aina tano za virai: virai nomino, virai vivumishi, virai vitenzi, virai vielezi na virai vihusishi. Kwa kila aina ya kirai mfano mmoja umetolewa. Mifano ya virai kutoka riwayani:

*Amani na Imani* walikuwa wamerejelea *kazi zao za awali* – kirai nomino (Kidagaa Kimemwozea).

*Yule paka maskini* akasagika vipande vipande *kwa kukokotwa barabaran* – Kirai kielezi (Kidagaa Kimemwozea).

Yeye alikuwa mtu *mwenye chake* – Kirai kivumishi (Chozi la Heri).

*Kilichobakia*ni tabasamu yake ya milele – Kirai kitenzi (Chozi la Heri).

Mtalichukua shamba langu *juu ya maiti yangu* – Kira*i* kihusishi (Kidagaa Kimwozea).

*Vishazi*

Massamba na wengine (1999) wakimnukuu Lyons wanasema kishazi ni kundi la maneno lenye kiima na kiarifa. Kwa mujibu wa mtafiti, kishazi ni fungu la maneno lenye kiima na kiarifa au kiarifa pekee. Kuna aina mbili kuu za vishazi; vishazi huru na vishazi tegemezi.

(a) Vishazi Huru

Vishazi huru ni vishazi vinavyojitegemea na havihitaji msaada wowote kutoka kwa vishazi vingine ili kutoa maana inayokusudiwa (Massamba na wengine, k.h.j). Mifano kutoka riwayani:

*Jua lilikuwa la utosini* (Kidagaa Kimemwozea).

Baada ya kurejea katika shughuli zake za kawaida kazini, *Mwangeka alitafuta kiwanja cha kujengea nyumba* (Chozi la Heri).

(b) Vishazi Tegemezi

Kishazi tegemezi ni kishazi ambacho hakiwezi kujitegemea katika kuwasilisha maana kamili. (Matinde, 2012). Mifano kutoka riwayani:

Ridhaa alikuwa na miaka kumi *alipohamia humu* (Chozi la Heri).

*Zahanati iliyokuwa Sokomoko* iliitwa Zahanati ya Nasaba Bora (Kidagaa Kimemwozea).

*Sentensi za Kiswahili Sanifu*

Sentensi ni neno au fungu la maneno lenye uarifishaji mkamilifu (Matinde, k.h.j). Sentensi ndicho kipashio kikubwa kuliko vipashio vingine katika lugha. Sentensi huweza kuundwa kwa kishazi kimoja ua zaidi. Kwa muijibu wa Matinde (k.h.j.), sentensi huainishwa kwa misingi ya vigezo viwili; kigezo cha kimuundo na kigezo cha kiuamilifu. Mtafiti alizingatia aina za sentensi kwa kutegemea muundo wake.Licha ya sentensi za Kiswahili kuainishwa kama tatu pekee, mtafiti ameainisha aina tano za sentensi nazo ni: sentensi sahili, sahili ambatani, changamani, sahili changamani na changamani ambatani

(a) Sentensi Sahili

Sentensi sahili ni sentensi ambayo imeundwa kwa kishazi huru kimoja ambacho maana yake ni kamilifu. Aidha sentensi hizi huwa na muundo wa kiima na kiarifa na huwa na wazo moja (Matinde, k.h.j). Kwa mujibu wa mtafiti, sentensi sahili ni sentensi yenye muundo wa kiima na kiarifa au kiarifa pekee na huwasilisha wazo moja.Mifano ya sentensi sahili kutoka riwayani:

*Hatung'atuki* (Chozi la Heri).

*Anamshukuru mungu kimoyomoyo* (Chozi la Heri).

*Bi. Zuhura alikihurumia kitoto hicho* (Kidagaa Kimemwozea).

(b) Sentensi Sahili Ambatani

Sentensi sahili ambatani ni sentensi ambayo ina vishazi viwili huru au zaidi vilivyounganishwa kwa kiunganishi na kiunganishi kikiondolewa kila kishazi hujisimamia kama sentensi (Massamba na wengine, k.h.j). Hata hivyo kuna sentensi sahili ambatani ambazo hazina kiunganishi.

Sentensi sahili ambatani zenye vishazi huru viwili na kuunganishi:

i. *Mama alitutoroka lakini moyoni nahisi yu hai* (Kidagaa Kimwozea).
ii. *Mama mtu alikuwa ameamua kwamba hapa hapamweki* (Chozi la Heri).

Mifano ya sentensi sahili ambatani ambazo hazina kiunganishi:

i. *Niligutuka tu, nimekiita hivyo* (Kidagaa Kimwozea).
ii. *Ninakumbuka, nilikuhadithia* (Kidagaa Kimwozea).

(c) Sentensi Changamani

Massamba na wenzake (k.h.j) na Matinde (k.h.j) wanafasili sentensi changamani kuwa ni sentensi ambayo huundwa kwa vishazi huru na vishazi tegemezi. Mifano kutoka riwayani:

i. *Zahanati iliyokuwa Sokomoko iliitwa Zahanati ya Nasaba Bora* (Kidagaa Kimwozea).

*Iliyokuwa Sokomoko* – **kishazi tegemezi.**

*Zahanati iliitwa Zahanati ya Nasaba Bora* – **kishazi huru.**

ii. *Baada ya kipigo hiki cha babake, Mwangeka aliapa kuajibika zaidi*. (Chozi la Heri)

*Baada ya kipigo hiki cha babake* – **kishazi tegemezi.**

*Mwangeka aliapa kuajibika Zaidi* – **kishazi huru.**

(d) Sentensi Sahili Changamani

Hizi ni sentesi ambazo zimeundwa kwa sentensi sahili na changamano.Mifano kutoka riwayani:

i. *Dadangu Lowela kaniambia kwamba atakuja nyumbani tu* **endapo** *sitafichua siri yake kwa wazazi wangu* (Kidagaa Kimemwozea).

ii. Hayo unayowazia siyo, **ila** naona ni muhimu nihamie ile nyumba yangu ya afueni (Chozi la Heri).

(e) Sentensi Changamani Ambatani

Hizi sentensi zimeundwa kwa sentensi mbili changamani na kuunganishwa kwa kiunganishi.

Mifano**:**

(i) *Kasri lake kubwa lilizungukwana ua uliopashwa kulengetwa kila juma,* **ingawa** *ulikuwa na matawi yaliyojizongomeza na kujitoa ovyo. (Kidagaa Kimwozea)*

(ii) *Utingo aliponiuliza tulikokuwa twaelekea, nilisita* **kwa kuwa** *sikujua* nilikokuwa *nikielekea.* (Chozi la Heri)

Kutokana na mifano iliyotolewa hapo juu, ni bayana kuwa riwaya inaweza kutumiwa kutoa muktadha wa ufafanuzi wa virai, vishazi na aina za sentensi.


**Utekelezaji wa Mwelekeo Mseto Katika Ufundishaji wa Muundo wa Sentensi kwa Kutumia Riwaya**

Lengo la pili lilikuwa kubaini utekelezaji wa mwelekeo mseto katika ufundishaji wa muundo wa sentensi kwa kutumia riwaya. Mtafiti katika kuafiki hili lengo alipaswa kujibu swali, je, walimu wanazingatia mwelekeo mseto katika ufundishaji wa muundo wa sentensi kwa kutumia riwaya? Mtafiti alisaili walimu na kutathmini stakabadhi za kitaaluma kama maazimio ya kazi au mipangilio ya masomo. Licha ya hayo, mtafiti alitathmini mitihani ili kubaini iwapo walitahini mindo ya sentensi kwa kutumia riwaya.

Matokeo yalionyesha kuwa ni walimu 24 (68.6%) hawakutambua pendekezo la K.I.E (2002) kuhusu usetaji wa fasihi na lugha. Walimu 11 kwa 35 (31.4%) walikuwa wanatambua pendekezo la silabasi ya K.I.E (2002) kuhusu usetaji wa fasihi na lugha. Walimu 7 kwa 11 (63.6%) ingawa walifahamu pendekezo hilo, walipata ugumu wa utekelezaji. Walimu 4 kwa 11 (36.4%) ndio waliotumia riwaya katika kufundisha vipengele vya lugha kama ifuatavyo; virai, walimu 3 kwa 4 (75%), vishazi, walimu 3 kwa 4 (75%), aina za sentensi, walimu 4 kwa 4 (100%); shamirisho, walimu 2 kwa 4 (50%); ufupisho, walimu 2 kwa 4 (50%); ufahamu, walimu 0 kwa 4(0%); msamiati, walimu 2 kwa 4 (50%), na uakifishaji, walimu 3 kwa 4 (75%). Kulingana na hayo matokeo walimu walifundisha aina za sentensi, vishazi, virai na uakifishaji kwa kutumia riwaya ukilinganisha na vipengele viningine vya lugha. Rejelea *Grafu ya 1*.

Licha ya walimu 4 kwa 11 (36.36%) kufundisha muundo wa sentensi kwa kutumia riwaya, hakukuwa na ithibati yoyote katika maazimio ya kazi na mipangilio ya masomo. Walimu walikiri kuwafafanulia wanafunzi miundo ya sentensi waliposoma riwaya wala si riwaya kutumiwa kufundisha muundo wa sentensi katika kipindi cha lugha. Maazimio ya kazi yaliandaliwa kulingana na silabasi na vitabu vya kiada wala si kwa kutumia riwaya pia. Isitoshe, hakuna mwalimu hata mmoja aliyeandaa maswali ya muundo wa sentensi katika mtihani kwa kutumia riwaya. Walioseta walitumia ushairi kama ufahamu na wengine kuweka fasihi simulizi katika sehemu ya isimujamii badala ya isimujamii au kuweka kuweka isimujamii na fasihi simulizi wakati mmoja. Walimu 31 (88.6%) ambao hawakuseta kwa njia yoyote walionyesha kuwa riwaya inaweza kutumiwa katika kufundisha muundo wa sentensi na kuandaa mtihani wa lugha.

*Grafu 1: Vipengele vya lugha ambavyo hufundishwa kwa kutumia riwaya*




Matokeo haya ya walimu yanawiana na ya wanafunzi ambapo wanafunzi 24 (55.8%) walikubali kuwa walimu huwafafanualia miundo ya sentensi wanaposoma riwaya. Kwa hivyo,


usetaji ambao umedhihirika ni ule wa kufundisha riwaya na muundo wa sentensi kwa pamoja wala si ufundishaji wa muundo wa sentensi kwa kutumia riwaya katika kipindi cha lugha. Aidha, matokeo yanaonyesha kuwa walimu walifafanua aina za sentensi katika riwaya sana (wanafunzi 21 (48.14%) zikifuatwa na vishazi (wanafunzi 15, 34.88%) na virai (wanafunzi 13, 30.23%) vikifuatwa na vipengele vingine vya muundo wa sentensi kwa asilimia kidogo; aina za maneno 8 (18.60%) na shamirisho 3 (6.98%). Rejelea *Jedwali la 1*:

*Jedwali 1: Vipengele vya muundo wa sentesi vinavyofundishwa kwa kutumia riwaya.*

| Vipengele vya muundo wa sentensi | Idadi ya wanafunzi | Asilimia |
|---|---|---|
| Aina za sentensi | 21 | 48.84% |
| Virai | 13 | 30.23% |
| Vishazi | 15 | 34.88% |
| Shamirisho | 3 | 6.98% |
| Aina za maneno | 8 | 18.60% |

Hata hivyo, ufundishaji huo kwa kutumia riwaya ulikuwa wa nadra (5, 11.63%). Matokeo yalionyesha kuwa walimu walitumia vitabu vya kiada sana (wanafunzi 43, 100%) na kutoa kichwani (wanafunzi 21, 48.84%). Matumizi ya tamthlia, fasihi simulizi na hadithi fupi zilichukua asilimia 2.33% mtawalia. Hata hivyo, ingawa riwaya haikutumika sana, ni ishara kuwa riwaya inaweza kutoa muktadha wa ufafanuzi wa muundo wa sentensi. Rejelea *grafu ya 2*:

*Grafu 2: Vitabu vinavyotumiwa katika ufundishaji wa muundo wa sentensi*




Ni dhahiri kuwa kuna haja ya walimu kuhamasishwa kuhusu ufundishaji mseto wa fasihi na lugha. Kwa hivyo, utafiti huu unaohusu matumizi ya riwaya katika kutoa muktadha wa ufafanuzi wa muundo wa sentensi utakuwa na manufaa kwa vile utatoa mwelekeo wa utekelezaji wa ufundishaji mseto wa muundo wa sentensi kwa kutumia riwaya.

**Hitimisho**

Kwa muhtasari, utafiti huu ulihusu matumizi ya riwaya katika kutoa muktadha wa ufafanuzi wa muundo wa sentensi na utekelezaji wake shuleni. Kutokana na matokeo, walimu wengi hawana ufahamu wa ufundishaji mseto.Wachache walio na ufahamuhuseta fasihi na vipengele vya lugha kwa nadra. Baadhi yao walifafanua muundo wa sentensi wakati waliposoma riwaya bali si kufundisha muundo wa sentensi katika kipindi cha lugha huku riwaya ikirejelewa. Aidha matumizi ya riwaya yalitumika kwa nadra. Walimu wengi walitumia vitabu vya kiada na mifano kutoka vichwani katika kufundisha muundo wa sentensi. Madai haya yameungwa mkono na Pekoz (2008) kuwa ufundishaji wa lugha pekee bado unawika. Hata hivyo, walimu wana ufahamu wa vipengele vya lugha vinavyoweza kufundishwa kwa kutumia riwaya. Mtafiti anapendekeza walimu waweze kuhamasishwa kuhusu ufundishaji wa mwelekeo mseto kupitia elimu ya vyuoni, semina na makongamano.Isitoshe, Taasisi ya Elimu ifanye mabadiliko katika mtaala na silabasi na vitabu vya kiada na vya ziada ili viweze kufaa mbinu hii mpya ya ufundishaji.

**MAREJELEO**


Aina, N.F. (1979). *Social Students for Primary School Teachers*. Oxford University Press.

Brendto, L.K. (1999). Maria Montessori: Teacher of unteacheable children. *Reclaiming children and youth.* 7(4), pp 201-204.

Brumfit, C. (1985). *Language and literature teaching: From practice to principle*. Oxford: Pergamon Press.

Brunfit, C.J. na Carter, R. A. (Eds) (1986). *Literature and Language Teaching.* Oxford: Oxford University Press.

Dewey, J. (1938). *Experience and Education.* New York: Macmillan

Good, C. (Ed) (1973). *Dictionary of Education.* Third Edition. New York: McGraw Hill.

Graham, M.A, (2007). Art, ecology and art education. Locating art education in critical place-based pedagogy, *Studies in Art Education,* 48(4), 375-391.

Hammerly, H. (1985). *An integrated theory of Language teaching and its practical consequences.* Blaine. Washington and Burnaby, B.C, Second Language Publications.

Khatib, M., Rezaei, S., na Derakhshan, A. (2011). Literature in EFL/ESL Classroom. *English Language Teaching*, *4*(1), 201-208.

K. I. E, (2002). Secondary *Education Syllabus*. Vol.1. Nairobi: K.I.E.

K.I.E, (2006). *Kiswahili Sekondari: Mwongozo wa Mwalimu*. Nairobi: K.I.E.

K.N.E.C. Examination Report, (2017). Languages: The Test Development Department. Vol.1

Kothari, C.R. na Garg, G. (2014). *Research Methodology: Methods and Techniques* (Third Edition). New Age International Printers.

Mamai, M. N. (2012). Utekelezaji wa Mwelekeo Mseto katika shule za upili nchini Kenya. Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde.

Massamba, D.P.B., Kihore Y.M. na Hokororo, J. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu* (SAMIKISA). Dar es Salaam: TUKI.

Matei, A.K. (2014). *Chozi la Heri.* One Planet Publishing and Media Services Limited.

Matei, A.K. (2011). *Fani ya Fasihi Simulizi kwa Shule za Upili*. Oxford University Press.

Matinde, R.S. (2012). *Dafina ya Lugha*, *Isimu na Nadharia.* Tanzania. Serengeti Educational Publishers.

Mckay, S. (1982). Literature in ESL Classroom. *TESSOL Quarterly*, (4), 529-534.

Montessori, M. (2013). A critical consideration of the new pedagogue in its relation to Modern Science.In D.J. Flinters and S.J. Thornto (ed.), *The Cirriculum Studies reader* (pp 19-32). New York: Routledge.

Moatei, M. (1948). *The Discovery of the Child*. Madras: Kalkshetra Publishing Press.

Opunde, S. (2012). Matumizi ya Riwaya katika Ufundishaji wa Ngeli za Kiswahili katika shule za Upili nchini Kenya. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia.

Pekoz, B. (2008). *Integrating Grammar for Communicative Language Teaching.* Retrieved September 15, 2010 from http://iteslj.org/Techniques/Pekoz.Grammar.html

Piaget. J. (1952). *The Original of Intelligence in Children.* New York. NY.W.W. Norton & Co.

Pigdon, K. na Wooley, M. (1992). *The Big Picture: Integrating Children's Learning*. Armadel. Vic: Eleanor Curtain Publishers

Republican of Kenya (1999). The Koech Report. Nairobi. Government Printers.

Republican of Kenya (1999). 8-4-4 Educational System.Nairobi. Government Printers.

Shang, H. (2006). *Content-based Instruction in the EFL Literature Curriculum.* Retrieved

September 15, 2010, from hppt://www edu tw/English.

Schiro, M.S. (2012). *Cirriculum theory: Conflicting visions and enduringconcerns* (2nd Ed.). Los Angeles: Sage Publications.

Shoemaker, B. (1989).*Integrative Education: A curriculum for the Twenty First Century*.Oregon School Study Council 33/2.

Walibora, K. (2012). *Kidagaa Kimemwozea*. Nairobi. Targets Publications Limited.

Wamitila, K.W. (2005).*Chemchemi za Kiswahili Kidato cha Tatu*. Nairobi. Focus mtindo wa asilimia.books Publishers.

Wamitila, K.W. (2003).*Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*.Nairobi.Focus Publishers Limited.